**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Syria**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Na: 08 / 1446 H | Alhamisi, 10 Jumada II 1446 H | 12/12/2024 M


## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

### Uvamizi wa Umbile la Kiyahudi na Mashambulizi Yake ya Kiadui kwenye Ardhi ya Ash-Sham

### Jinai zinazoendelea ambazo ni Utawala wa Uislamu na Dola Yake ya Khilafah Pekee ndio Unaoweza Kusitisha na Kuvunja Nguvu yao

**(Imetafsiriwa)**

Tangu kuanguka kwa dhalimu Assad mnamo tarehe nane mwezi huu, makundi ya umbile la Kiyahudi yamekuwa yakishambulia ardhi ya Ash-Sham, na ndege zake zimekuwa zikivamia anga yake kwa mashambulizi ya angani yenye nia mbaya ambayo yalilenga miji kadhaa, na maeneo ya kijeshi. Mashambulizi haya yamefika katika mji wa Deir ez-Zor mashariki mwa Syria. Mashambulizi hayo ya chuki na kihalifu yamejikita kwenye maghala ya silaha, vikosi vya ulinzi wa anga katika maeneo ya kati na kusini, vituo vya utafiti wa kisayansi wa kijeshi, na viwanja vya ndege vya kijeshi, ikiwa ni pamoja na uwanja wa ndege wa kijeshi wa Al-Mazzeh viungani mwa Damascus.

Mnamo siku ya Jumanne, 10/12/2024, jeshi la umbile hilo lilifichua “utekelezaji wake wa mashambulizi ya anga dhidi ya karibu 80% ya uwezo wa kijeshi wa Syria, katika mojawapo ya operesheni kali zaidi za mashambulizi ya Jeshi la Anga la ‘Israel’.”

Uvamizi wa kijeshi wa umbile hilo kusini mwa Syria umefikia takriban kilomita 25 kusini magharibi mwa mji mkuu, Damascus. Ramani zimeonyesha jeshi la umbile la Kiyahudi likichukua udhibiti wa kilele cha Mlima Hermon, pamoja na vijiji na miji kadhaa ndani ya eneo lisilo na jeshi, na kupenya hadi kilomita 18 ndani ya ardhi ya Syria. Redio ya umbile hilo iliripoti kwamba “ndege za kivita 350 zilishambulia maeneo kutoka Damascus hadi Tartus, na kuharibu makumi ya ndege, kambi za kijeshi, mifumo ya ulinzi wa anga na maghala ya silaha.” Netanyahu alionya akisema: “Iwapo utawala huu utairuhusu Iran kuregesha uwepo wake nchini Syria, kuruhusu uhamisho wa silaha za Iran au silaha nyingine zozote kwa Hezbollah, au kutushambulia, tutajibu kwa nguvu na kutia gharama kubwa. kilichoukumba utawala uliopita kitaukumba huu pia.” Wakati huo huo, waziri wa ulinzi wa uvamizi huo, Yisrael Katz, alisema kuwa makombora ya jeshi la wanamaji la ‘Israel’ yaliharibu meli za wanamaji wa Syria, na kuongeza kuwa majeshi ya ‘Israel’ yamewekwa katika eneo la kudumisha usalama (buffer) kati ya Syria na Milima ya Golan.” Pia aliamuru kuanzishwa kwa “eneo tasa la ulinzi” kusini mwa Syria “bila uwepo wa kudumu wa Israel ili kuzuia tishio lolote la kigaidi kwa 'Israel'.” Netanyahu alithibitisha zaidi mnamo Disemba 8, 2024, “kuvunjika kwa makubaliano ya kujiondoa” na Syria, yaliyotiwa saini mwaka 1974. Alitangaza kwamba sehemu ya Milima ya Golan ya Syria inayokaliwa na kushikiliwa na umbile la Kiyahudi “itabakia ya ‘Israel’ milele.”

Hili ndilo umbile la Kiyahudi, lililofanya mauaji baada ya mauaji mjini Gaza na maeneo mwenza yake, ikiyamiminia mabomu yake, moto, na makombora kutoka kwa ndege zake, chini ya usaidizi usio na kikomo wa Amerika. Hiki ndicho kiburi chake bila kuwepo mtu yeyote wa kukizuia na kuvunja nguvu zake.

Jinai hizi ovu zinalenga silaha zote za kimkakati nchini Syria, kwa hofu kwamba zinaweza kuangukia mikononi mwa wale ambao wangezitumia ipasavyo na kwa mwelekeo sahihi. Lengo lao ni kuiacha Syria ikiwa imevunjika na kutokuwa na nguvu, isiweze kung'oa umbile hili au hata kuleta tishio tu kwake. Wanataka Syria ya baadaye iwe dola dhaifu, inayonyenyekea, na dhalilifu, isiyo na silaha wala nguvu za kutegemea. Ndio, hivi ndivyo Amerika na wafuasi wake, umbile la Kiyahudi, wanachotamani. Ndege zenye uadui huvamia kwa uhuru bila jibu lolote—hata kauli ya kulaani au kupinga kutoka kwa wale waliojitwalia uongozi baada ya magofu ya dhalimu Assad, wakinyamaza kimya kama kaburi. Badala yake, wanatoa hakikisho kwamba hakuna nia ya vita vyovyote vya nje katika siku zijazo, baada ya dhalimu anayekimbia Assad kuweka “haki ya kujibu” huku akifurahia “uvumilivu wake wa kimkakati” na kutoa taarifa za kulaani na malalamiko kwa jumuiya ya kimataifa, mshirika wa utawala wa zamani na umbile la Kiyahudi katika vita vyetu.

Tuna yakini kwamba kiburi cha Mayahudi kitaendelea, na hakitasitishwa isipokuwa na wanaume wa Dola ya Kiislamu, Dola ya Khilafah ambayo inatakiwa kusimamishwa na ni faradhi juu yetu sote kuleta kuwepo wake. Dola inayoongozwa na Waumini wema, walio huru na walio safi, wasiomuogopa yeyote ila Mwenyezi Mungu, kwa kutaka kujikurubisha Kwake kwa kupigana na umbile la Kiyahudi, kuvunja nguvu zake, na kugeuza kiburi chake na vitimbi dhidi yake, na kulitowesha bila ya kusaza mabaki yake, hivi karibuni, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Tunatoa wito kwa wanamapinduzi na mujahidina walio huru katika ardhi ya Ash-Sham, waliomuangusha dhalimu wa Ash-Sham baada ya kudhihirisha matendo ya ajabu ya ushujaa na ujasiri wa ajabu, wasiwe kama yule anayetengua uzi wake baada ya kwisha kuusokota kwa nguvu, lakini kuchukua msimamo thabiti na kusonga kuelekea kwenye kusimamisha Dola ya Uislamu. Hebu na tujipatie radhi na usuhuba wa Mwenyezi Mungu, tukionyesha shukrani za kweli kwa ushindi aliotubariki nao. Sifa na shukrani zetu kwa Mwenyezi Mungu zinapaswa kudhihirika katika kuhukumu kwa Shariah Yake na kusimamisha dola yake juu ya magofu ya utawala wa kisekula ulioondoka.

Hapo ndipo pekee umbile la Kiyahudi na wale walio nyuma yake miongoni mwa makafiri na wahalifu wa ulimwengu huu watajua mapigano na upinzani ni kitu gani. Wakati huo, tutatimiza maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**[قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُّؤْمِنِينَ]**

**“Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini”** [At-Tawba:14].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**katika Wilayah Syria**


للتواصل معنا:
Skype: TahrirSyria
media@tahrir-syria.info
syriatahrir44@gmail.com
+905350370863 واتس

المكتب الإعلامي على تويتر
https://twitter.com/AttahrirSyria
المكتب الإعلامي على التليغرام
https://t.me/syriatahrir

المكتب الإعلامي المركزي
www.hizb-ut-tahrir.info
المكتب الإعلامي في سوريا
www.tahrir-syria.info